**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Kenya**

بسم الله الرحمن الرحيم

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

**Toleo: 1446/02 H** | **Jumatano, 22 Rabi' I 1446 H** | **25/09/2024 M**

**<u>Taarifa kwa Vyombo Vya Habari</u>**

# Muozo wa Tabia na Maadili, Tunda la Mfumo Mbovu wa Ubepari

**(Imetafsiriwa)**

Kutekwa nyara kwa mwanablogu wa Mombasa Bruce John, ambaye pia alilawitiwa na kundi la wanaume kumezua kilio cha umma katika Jiji la Pwani la Mombasa na Kenya kwa jumla. Wito wa haki umekuwa mwangwi, marafiki, familia, na wanaharakati wa haki za binadamu wakikusanyika kumuunga mkono mwanablogu huyo mchanga. Sisi katika **Hizb ut Tahrir / Kenya** tungependa kutaja yafuatayo:

Inatia wasiwasi mkubwa kwamba muozo na tabia mbaya imefikia kiwango cha kutisha kwa katika mizani ya kimataifa. Maadili ya kiliberali ya kisekula yameunda umma kwa jumla katika kutabanni mbinu chafu kama vile unyanyasaji na kashfa kama zana za kuonyesha chuki za kisiasa.

Ulimwenguni kote, ni ukweli uliodhihirika kwamba ubakaji na ulawiti vimekuwa zana ya kisiasa na kijeshi ya kudhibiti chuki za kisiasa. Hata hivyo hii inapaswa kuwakumbusha wanadamu kwa jumla na Umma wa Kiislamu hususan kufilisika tabia na maadili ya itikadi ya kisekula ambayo haina mwelekeo na maadili. Tofauti na Uislamu, Usekula huvua maadili yake kutoka katika falsafa ya starehe (utilitarianism) ambayo hupigia debe vitendo vinavyokuza furaha au raha na kupinga vitendo vinavyosababisha kutokuwa na furaha au madhara vinapoelekezwa kwenye kufanya maamuzi ya kijamii, kiuchumi, au kisiasa. Wanadamu chini ya jamii ya kibepari isiyo na maadili wamekuwa wabaya zaidi kuliko wanyama kama ilivyoelezwa katika Quran:

[ثُمَّ رَدَدْنَاهُ أَسْفَلَ سَافِلِينَ] **"Kisha tukamrudisha kuwa chini kuliko walio chini!"** [At-Tiin: 05].

Kwa zaidi ya karne 13, Uislamu tangu kuasisiwa kwa Dola mjini Madina hadi kuvunjwa kwake na Wakoloni wa Magharibi mnamo 1924, wanadamu walikuwa na viwango vya juu vya maadili. Hili lilidhihirika kwa kuegemea kwenye itikadi ya Kiislamu ambayo inalinda na kulea maadili yenye malengo na hivyo kudhamini mafanikio katika nyanja zote za maisha. Ni dhahiri, Uislamu ni hitaji la wakati sasa kuliko wakati mwingine wowote katika historia ili kunyanyua maadili ya kimalengo ya jamii. Mwenyezi Mungu (swt) asema:

[وَلَقَدْ كَرَّمْنَا بَنِي آدَمَ وَحَمَلْنَاهُمْ فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ وَرَزَقْنَاهُم مِّنَ الطَّيِّبَاتِ وَفَضَّلْنَاهُمْ عَلَى كَثِيرٍ مِّمَّنْ خَلَقْنَا تَفْضِيلاً]

**"Na hakika tumewatukuza wanaadamu, na tumewapa vya kupanda nchi kavu na baharini, na tumewaruzuku vitu vizuri vizuri, na tumewafadhilisha kwa fadhila kubwa kuliko wengi miongoni mwa tulio waumba."** [Al-Isra'a: 70].

**Shabani Mwalimu**

**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari wa Hizb ut Tahrir**

**Kenya**